

**MKATABA WA KWENDA MASOMONI**

**KATI YA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA NYASA**

**NA**

.....

**UMETAYARISHWA NA**  
**KITENGO CHA SHERIA,**  
**P.O.BOX.90**  
**MBAMBA-BAY,NYASA.**

## **MKATABA WA KWENDA MASOMONI**

Makubaliano haya yanafanyika leo tarehe ..... mwezi ..... mwaka 20...

### **KATI YA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA NYASA**, Sanduku la Posta 90, Mbamba-Bay, NYASA, Tanzania. ambaye katika Mkataba huu atajulikana kama **Mwajiri** kwa upande mmoja.

### **NA**

..... wa Sanduku la Posta ....., Tanzania ambaye atajulikana kama **Mwajiriwa** kwa upande mwingine.

**Mwajiriwa** kwa hiyari yake anaomba kwenda masomoni kwa ruhusa ya mwajiri wake, na **mwajiri** ameridhia na kumruhusu mwajiriwa kwenda masomoni.

**HIVYO BASI**, Pande zote mbili kwa pamoja zinakubaliana kama ifuatavyo;

1. Kwamba, endapo mwajiriwa anataka kujisomesha mwenyewe basi, mwajiri yeye atahusika kutoa ruhusa tuu pale atakapona inafaa kulingana na uhitaji wa mwajiriwa katika nafasi ya kazi yake.
2. Kwamba, mwajiriwa atajigharimia gharama zote za masomo kama barua yake ya tarehe....., 20..... ya kuruhusiwa kwenda masomoni inavojieleza.
3. Kwamba, gharama za masomo ni kama zifuatazo usajili wa kujiunga na chuo, ada ya mitihani, usafiri, michango ya chama cha wanafunzi, mahitaji maalumu ya kitivo na vazi rasmi la kuhitimu (joho) na gharama zingine zinazoweza kujitokeza zinazu husu masomo yake.
4. Kwamba, ili mwajiriwa kupata nafasi ya kwenda shule lazima awe ameitumikia ajira yake kwa muda wa miaka mitatu (3) baada ya kuthibitishwa kazini na awe ameitumikia Halmashauri ya Nyasa kwa kipindi hicho.
5. Kwamba, mwajiriwa awe ametimiza sifa zinazohitajika kwenda masomoni, sifa ambazo zitamruhusu kwenda kuongeza elimu yake.
6. Kwamba, mwajiri anao uhuru wa kutoa au kutotoa ruhusa kwa mwajiriwa kulingana na uhitaji wa kitengo ambacho mwajiriwa anatoka.
7. Kwamba, mwajiriwa hatoruhusiwa kuendelea na masomo ya juu zaidi ya ombi la mwanzo aliloomba.

8. Kwamba, mwajiriwa baada ya kumaliza muda wa masomo arudi na kuripoti kwa mwajiri na kuitumikia elimu aliyopata kwanza.
9. Kwamba, kwa mwajiriwa atakaye endelea na masomo zaidi ya ombi aliloruhusiwa katika mkataba huu basi atachukuliwa hatua za kinidhamu.
10. Kwamba, mwajiriwa atakayetoka masomoni kabla ya muda wake atatakiwa kuandika barua kwa mwajiriwa akitoa sababu ya kutoka masomoni kabla ya muda.
11. Kwamba, mwajiriwa ambaye atafukuzwa au kufeli shule kutokana na uzembe wake, Mwajiri baada ya kulithibitisha hilo anaweza kumfutia ruhusa mwajiriwa na kumtaka aludishe ada/gharama ambazo mwajiri amemchangia mpaka kufikia muda anafukuzwa shule kama mwajiri atakuwa amechangia gharama za Masomo.
12. Kwamba, mwajiriwa anatakiwa kujiendeleza kwenye taaluma yake tuu kulingana na barua yake ya ruhusa ya kwenda masomoni, na kutoka nje ya taaluma yake ni kosa la kumdanganya mwajiri.
13. Kwamba, endapo mwajiriwa atabadilisha taaluma yake pindi atakapofika shuleni basi atachukuliwa hatua za kinidhamu kwa kumdanganya mwajiri wake ikiwa ni pamoja na kumfutia ruhusa..
14. Kwamba, endapo mwajiriwa ataamua kwa ridhaa yake kuacha katikati ya masomo basi hatua kali za kinidhamu zitachukuliwa dhidi yake.
15. Kwamba, endapo mwajiriwa kwa sababu za kiafya atashindwa kuendelea na masoma basi, mwajiri atawasiliana na chuo husika ili kuweza kuilinda nafasi hiyo mpaka atakaporudia kwenye afya yake, na kutakiwa kurudi masomoni tena.
16. Kwamba, mwajiriwa atatakiwa kufanya yafuatayo kabla ya kwenda masomoni;
  1. Kujaza na kusaini mkataba huu
  2. kukabidhi ofisi na kuleta uthibitisho wa makabidhiano kwa mwajiri.
17. Mwajiriwa endapo ataghairi kwenda masomoni baada ya kusaini mkataba huu basi atatakiwa kumpa taarifa mwajiri ndani ya siku saba (7).
18. Kwamba, mwajiriwa atatakiwa kuleta matokeo yake ya kila muhula wa masomo kwa mwajiri ili kujiridhisha na maendeleo ya mwajiriwa chuoni kitaaluma.
19. Kwamba, mkataba huu unalindwa na sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**HIVYO BASI** pande zote mbili katika mkataba huu wanakubaliana na kutia saini katika, tarehe, mwezi na mwaka kama inavyoonekana chini.

**UMESAINIWA na KUWASILISHWA na  
HALMASHAURI YA WILAYA YA NYASA**

Leo tarehe.....mwezi ..... 20...

**MUHURI**

**SAINI .....**

**JINA:JIMSON P. MHAGAMA**

**ANUANI: 90 MBAMBA BAY,  
RUVUMA.**

**CHEO: MKURUGENZI MTENDAJI(W)**

**SAINI .....**

**JINA:LISTON G.MOYO**

**ANUANI: 90 MBAMBA BAY,  
RUVUMA.**

**CHEO: AFISA UTUMISHI(W)**

**SAINI .....**

**JINA: .....**

**ANUANI: 90 MBAMBA BAY,  
RUVUMA.**

**CHEO: MWANASHERIA HALMASHAURI YA (W) NYASA**

**UMESAINIWA na KUWASILISHWA na**

.....  
Leo tarehe..... mwezi ..... 20....

.....  
**MWAJIRIWA**